
United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization



# Viongozi wa Dini:

## FAHAMU ZAIDI kuhusu CSE na Huduma Rafiki za Vijana!

***Mustakabali bora, wenye afya kwa vijana!***

Viongozi wa dini wana ustawi wa jamii zao katika moyo. Elimu ya kina ya Ujinsia, afya ya uzazi, maadili ya afya na stadi za maisha (CSE) ni taarifa ya kiutamaduni na inayofaa kulingana na umri ambayo inawafundisha vijana kuhusu masuala ya ujinsia, uhusiano na afya ya uzazi.

Ushahidi unaonyesha kwamba CSE inaongeza elimu ya watoto kuhusu VVU, inawasaidia kuchelewa kufanya ngono, kupunguza idadi ya wenzi wa kingono walionao na kuongeza elimu yao na matumizi ya kingamimba wanapotaka kuzuia maambukizo kwa ngono (STIs) na VVU, pamoja na mimba za utotoni.

***Unga mkono CSE - Saidia viongozi wetu wa baadaye!***

## Kwa nini CSE na Huduma rafiki za Vijana Vinakwenda Pamoja?

Elimu ya ujinsia, afya ya uzazi, maadili ya afya na stadi za maisha (CSE) inahitaji kuungwa mkono kwa taarifa na huduma za afya zinazopatikana, zinazowezekana kumudu na zinazofaa. Vijana na jamii zao wanakuwa katika hatari bila ya bidhaa ambazo zinawasaidia, ikiwemo: kondomu, kingamimba za kisasa, matibabu ya VVU na maambukizo kwa ngono, ushauri kuhusu mimba na matunzo na huduma nyingine. Hii ndiyo maana kujumuisha CSE katika shule na huduma rafiki kwa vijana katika jamii ni njia ya kuimarisha afya kwa muda mrefu kwa nchi za ukanda wa mashariki na kusini mwa Afrika.

## Huduma Rafiki kwa Vijana na Afya ya Uzazi ni Nini (YFS)?

Huduma rafiki kwa vijana na afya ya uzazi zinazingatia uelewa wa kina wa nini ambacho vijana katika jamii yoyote ile au jumuiya wanakitaka na kukihitaji. Zinahusisha afya ya uzazi ya vijana, haki na utofauti.

YFS zinajumuisha:

- Unasihi wa ujinsia na afya ya uzazi.
- Unasihi wa uhusiano na ujinsia.
- Unasihi wa unyanyasaji wa kingono.
- Unasihi kuhusu kingamimba na utoaji wa kingamimba, zikiwemo kingamimba za dharura.
- Kuzuia maambukizo kwa ngono (ikiwa ni pamojana VVU), huduma za upimaji na unasihi.
- Huduma za kutoa mimba (pale ambapo inaruhusiwa kisheria).
- Huduma za kabla na baada ya kujifungua.

*Ujinsia na afya ya uzazi vinasaidiwa na elimu, ujuzi na uwezo wa kufanya uchaguzi wa uwajibikaji, mzuri na kwa kuwa na taarifa kamili na salama za ujinsia — ikiwa ni pamoja na kuamua KUTOFANYA ngono.*

## Kwa nini viongozi wa dini wanapaswa kujihusisha na kusaidia CSE?

Baadhi ya watu wanahisi kwamba CSE inapingana na mafundisho ya dini, maadili na mafundisho na kwamba inaondoa tabia nzuri ya mtoto, lakini takwimu kuhusu mimba za utotoni katika Afrika zinathibitisha kwamba vijana tayari wanafanya ngono. Wakati wazazi na jamii wanazuia upatikanaji wa taarifa, watoto watatafuta vyanzo vingine. Siku hizi kuna vyanzo vingi. Hii ina maana watoto wanaweza kupata taarifa zisizo sahihi kuhusu masuala yanayohusu ujinsia na uhusiano, zinazowaweka hatarini.

Kama watu wa kiroho, ujinsia ni kipengele muhimu cha binadamu; kiroho na kijinsia vinasaidia kubadilisha tabia zetu. Elimu ni kipengele muhimu katika kuhakikisha maisha yenye afya.

*"Kutafuta elimu ni wajibu wa kila Muislamu, mwanamume na mwanamke."*
**– hadithi za Mtume Muhammad (SAW), kama zilivyoripotiwa na Ibn Maajah (Al Albaani: Saheeh)**

Kwa kutengeneza uhusiano mzuri kati ya utoaji wa CSE na YFS katika jamii na maadili ya dini, unaweza:

- Kuwahakikishia walimu na wanajamii kwamba utoaji wa CSE kwa watoto na vijana unaendana na maadili na kanuni ambapo wanatafuta kuishi.
- Kuwahakikishia wazazi kwamba huduma za ujinsia na afya ya uzazi kwa vijana (huduma rafiki kwa vijana) zinahakikisha afya nzuri ya vijana.
- Kuwasaidia watu wazima na vijana kukubali maadili ya elimu ya kina ya ujinsia, afya ya uzazi, maadili ya afya na stadi za maisha (CSE).

*Wajibu wa mchungaji, imamu au kiongozi mwingine wa dini sio kuwahukumu vijana bali kuwapa matumaini, upendo, matunzo na msaada wa kiroho!*

## Nini wajibu wangu kama kiongozi wa dini?

***Kufahamu mambo:*** Viongozi wa dini wanahitaji kufahamu mambo mapya kuhusu masuala yanayowakabili waumini wao. Mtu mmoja kati ya watatu mashariki na kusini mwa Afrika ana umri wa miaka 10–24 na 40% ya vijana hao hawana elimu ya kutosha kuhusu Virus vya UKIMWI (VVU).

***Kusaidia vijana kupata taarifa, matibabu na matunzo:*** Huduma rafiki kwa vijana zinahitajika kwa vijana wote, iwe ni waamilifu kingono au la. Huduma rafiki kwa vijana inamaanisha kutoa ushauri kuhusu kuacha kabisa kufanya ngono na kuwa na uhusiano na ukaribu kwa afya bila ya kufanya ngono. Sio kwa ajili ya vijana walio amilifu kingono tu. Taarifa sahihi zinazotoka moja kwa moja kwa watoa huduma ya afya zinaweza kuwa na matokeo mazuri sana katika kuhimiza tabia ya afya ya vijana.

***Viongozi wanawalinda wote:*** Ni wajibu wako kuhakikisha kwamba haki zote za watoto na vijana zinaungwa mkono ili waweze kufanya maamuzi kwa kuwa na taarifa na kwa kuwajibika na kuishi kwa afya, uzazi na maisha yenye ukamilifu.

***Zungumza:*** Watu wanakutafuta kupata mwongozo na uongozi kuhusiana na namna CSE katika shule na YFS katika jamii zinavyoendana na mafundisho ya dini. Vijana ni mustakabli wetu – wasaidie.

## Mithali 22:6

*Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mzee...*

*– Toleo Jipya la Kimataifa*

## Nifanye nini?

- ***Shirikisha vipengele vizuri vya CSE*** na jinsi vinavyoendana na mafundisho na maadili ya dini – toa kama barua kwa jamii na katika mahubiri yako na mafundisho mengine.
- ***Eleza kwamba CSE na YFS vinahimiza kuacha kufanya ngono*** kama mbinu ya awali na inayofaa ya ngono salama. Hata hivyo, programu za CSE ambazo zinahimiza kuacha kufanya ngono tu na hazishirikishi taarifa za uchaguzi mwingine, zimeonekana kufaa kwa kiasi kidogo katika kuhimiza afya, tabia ya kuwajibika kwa watoto na vijana.
- ***Saidia klabu za CSE katika vituo vya dini*** na tafuta njia za kujumuisha elimu ya tabia ya kuwajibika kwa watoto na vijana kwa pamoja na elimu ya dini – kwa njia hii unaweza kusaidia kuwafikia vijana ambao hawawezi kufikiwa kupitia shule au klabu za CSE. Husisha shule ili kuhakikisha nyote mnazungumzia kitu kinachofanana.
- ***Anzisha vipindi vya unasihi wa pamoja na shule na wafanyakazi wa afya wa kliniki kuhusu ukuaji,*** pamoja na katika mafundisho ya shule za Jumapili, madrasa, madarasa ya ubatizo au fursa nyingine.

***Watoto na Vijana Waliopewa taarifa:***
***Uchaguzi wenye uelewa – Unaweza Kuongoza Njia!***

UNESCO United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
SWEDEN
Norad
SAfAIDS Knowledge for action: The power to make a difference!

**Ofisi ya Kanda ya SAfAIDS, Zimbabwe**:
Barabara ya 17 Beveridge, Avondale, S.L.P A509, Avondale, Harare, Zimbabwe
Simu: +263 4 336 193/4, Faksi: +263 4 336 195
**Tovuti: www.safaids.net**